**OFISIYA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**

**MTIHANI WA KUFUNGA MWAKA 2024**

**KIDATO CHA KWANZA**

**KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2:30**

MAEELEKEZO.

i) Karatasi hii inasehemu A,B na C zenye jumla ya maswali (10).
ii) Jibu maswali yote.
iii) Sehemu A na C zina alama (15) kila moja na sehemu B ina alama (70)
iv) Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa blue au mweusi.
v) Vifaa vyote vya mawasiliano havitakiwi katika chumba cha upimaji.
vi) Andika namba yako ya upimaji katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| **NAMBA** | **ALAMA** |
|---|---|
| **1.** | |
| **2.** | |
| **3.** | |
| **4.** | |
| **5.** | |
| **6.** | |
| **7.** | |
| **8.** | |
| **9.** | |
| **10.** | |
| **Jumla** | |

**SEHEMU A: (alama 15)**

1. Katika vipengele (i) –(x) chagua herufi ya jibu sahihi.

i. Kila lugha katika mawasiliano hutumia mfumo ili mawasiliano yaeleweke. Miongoni mwa maneno yafuatayo, chagua mfumo ulio sahihi katika kuwasiliana.

A. Lugha, mawasiliano, ujumbe, mtoa ujumbe, media, mpokeaji na mrejesho.
B. Mpokea ujumbe, ujumbe, mawasiliano na mrejesho.
C. Mtoa ujumbe, ujumbe, media, mpokea ujumbe na mrejesho.
D. Media, mpokeaji, mrejesho, ujumbe na mtoaji.

ii. Zifuatazo ni dhima za lugha katika mawasiliano kasoro:

A. Kutambulisha utamaduni.
B. Kupashana habari.
C. Kutunza historia.
D. Kukaa maneno.

iii. Kiimbo hufasiliwa katika mazungumzo kuwa

A. Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji.
B. Mawimbi ya sauti wakati wa kuzungumza.
C. Kuzungumza kwa kutumia mawimbi ya sauti.
D. Yote hapo juu ni sawa.

iv. Chagua sentensi moja kati ya hizi zifuatazo kuwa haina maana zaidi ya moja :

A. Nipe sahani ya kulia.
B. Kaka amefua nguo.
C. Jenro amenunua mbuzi.
D. Mama ana kanga.

v. Dhana ipi kati ya hizi zifuatazo huonesha utambulisho wa mzungumzaji :

A. Sauti.
B. Silabi.
C. Matamshi.
D. Lafudhi.

vi. Mpira upo chini ya mti. Neno chini ya ni aina gani ya neno ?

A. Kitenzi kishirikishi.
B. Kivumishi.
C. Kihusishi.
D. Kiunganishi.

vii. Kila aina ya tangazo hutolewa na mtangazaji, wasikilizaji hupata habari kutoka kwa mtangazaji. Je, katika fasihi kazi hiyo huwasilishwa na nani kati ya hawa wafuatao :

A. Wasikilizaji.
B. Fanani.
C. Waandishi.
D. Wazungumzaji.

viii. Taja tofauti ya msingi kati ya mashairi na ngonjera :

A. Mpangilio wa maneno.
B. Mpangilio wa vina na mizani.

C. Mpangilio wa kimziki na kiridhimu.
D. Majibizano baina ya watu wawili au zaidi.

ix. Mtunzi wa kazi ya fasihi hujitahidi kufikisha mawazo makuu kwa walengwa kwa njia ya;

A. Dhamira.
B. Maudhui.
C. Falsafa
D. Fani.

x. Katika uhalisia unaomtofautisha muwasilishaji wa kazi za fasihi na mwingine huwa katika kigezo cha:

A. Maudhui.
B. Fani.
C. Mtindo.
D. Muundo.

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha maneno katika orodha "A" kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka B

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Soga<br>ii. Methali<br>iii. Tarihi<br>iv. Hadithi<br>v. visasili | A. Husimulia matukio mbalimbali ya kihistoria.<br>B. Husimulia picha ana mafumbo zinazoonesha ukinzani wa fikra au tukio.<br>C. Huonesha pande mbili zenye fikra katika usimuliaji kwa kutoa hekima na busara.<br>D. Husimuliwa kwa nia ya kufurahisha na kukejeli.<br>E. Husimulia vyanzo na asili ya jambo au kitu Fulani.<br>F. Ni masimulizi marefu yanayohusisha visa na matukio. |

3. Soma habari ifuatayo kasha jibu maswali

Miaka thelathini ya uhuru wa Tanganyika ilileta mabadiliko.Yalikuja mengi yakadharaulika na kusahaulika, kasoro la mageuzi . Oooo..! ulishika kwa uhakika . Mijadala ikawa tele tele. watu walisema wakasema . Si ghalibu watu kupata nafasi ya kutoa pumzi za ukweli, basi wakasema. Wengi walihofu mageuzi ya fujo.

Wakayakataa kwa nguvu zote. Wanamageuzi wakaja juu kama moshi wa vifuu vya nazi. Wakatetea uhuru na haki bila vikwazo. Chama kimoja hakitendi haki, kinalala bila mpango. Huu ukawa ndio msimamo walioubeba mgongoni na mabegani . kauli zao zilichoma akilini kama miiba kidondani na kuchonyota kama upupu mwilini.

Hatimaye, mwafaka ulipatikana, vyama vingi karibuni Tanzania ! waungwana wakashikana mikono kuonesha amani . wengine walilaani tume. Walisema tume ilitumia fedha ambazo zingetumiwa kwa shughuli za maendeleo. Walidai kuwa hapakuwa na lazima ya kugharimia tume ili iwaulize wananchi kuwa wanataka haki zao au la!

MASWALI

Chagua jibu sahihi

i) Waungwana walishikana mikono ili iweje?
- a) Kuleta vyama vingi
- b) Kutoa fujo
- c) Kuonesha amani
- d) Uhuru wetu uje

ii) Uhuru wa Tanganyika ulileta kwa miaka mingapi?
- a) Hamsini
- b) Kumi
- c) Thelathini
- d) Selasini

iii) Ili kuleta uhuru watu waliogopa mageuzi gani
- a) Ya furaha
- b) Ya huzuni
- c) Ya fujo
- d) Ya umoja

iv) Wanamageuzi walikuja juu kama nini?
- a) Moshi wa kuni
- b) Moshi wa nazi
- c) Moshi wa vifuu vya nazi
- d) Moshi wa nyasi

v) Msimamo wakati wa kudai uhuru ulibebwa wapi?
- a) Mabegani
- b) Mabegani na mgogoni
- c) Kichwani
- d) Mikononi

vi) Chama kimoja hakitendi haki, kina lala bila mpangilio kauli hii ilisemwa na?
- a) Watanganyika
- b) Wanamapinduzi
- c) Wakoloni
- d) Wanamageuzi

vii) Kauli za wapinzani zilifanyaje mwilini?
   a) Zilichoma
   b) Ziliumiza
   c) Zilifurahisha
   d) Zilichonyota

viii) Je hatima ya vyama ilikuwaje Tanzania?
   a) Vyama vingi vilikaribishwa Tanzania
   b) Vyama vingi vilifukuzwa
   c) Vyama vingi havikudumu
   d) Vyama vingi havipo

ix) Kwa nini tume ililaumiwa
   a) Kwa sababu ilitumia fedha
   b) Ilileta fujo
   c) Ilichochea matabaka
   d) Haikutetea juu ya uhuru

x) Baadhi wanasema tume ilitakiwa afanyeje?
   a) Kuuliza wananchi kama wanataka haki
   b) Isishilikishwe kabisa
   c) Itoe fedha za maendeleo
   d) Ikimbize wakoloni

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

4. Andika ‘K ‘ kwa kisemo cha kweli na ‘S’ kwa kisemo kisicho cha kweli kwenye sentensi zifuatazo
   i. Mrejesho wa ujumbe ni miongoni mwa vipengele vinavyotumikakatika mchakato wa mawasiliano________________________
   ii. ‘Mpendwa mama shikamoo, wote wazima?’ Hii ni sentensi inayotambulisha salamu au mwanzo wa barua ya kirafiki________________________
   iii. Redio ni kifaa kimojawapo kati ya vifaa visivyo toa taarifa katika jamii_________________
   iv. Ufahamu wa kuona ni kati ya aina za ufahamu katika lugha ya Kiswahili_____________
   v. La kuvunda lina ubani ____________________________
   vi. Mwenye kukataa pema, pabaya hapamkonyezi_________________
   vii. Lugha huweza kumtambulisha mtu_________________________
   viii. Mantiki ni umbo la ndani la kazi ya fasihi_____________________
   ix. Si lazima kuandika tarehe katika barua ya kirafiki____________________
   x. Kamusi hutumika kuhifadhi msamiati wa lugha ________________________

5. Eleza kwa mifano tofauti iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo.
   i. Uwasilishaji
   ii. Gharama
   iii. Ukubwa wa hadhira

iv. Idadi ya tanzu

v. Upokeaji wa mabadiliko

| Fasihi simulizi | Fasihi andishi |
|---|---|
| i. | i. |
| ii. | ii. |
| iii. | iii. |
| iv. | iv. |
| v. | v. |

6. Kwa kuzingatia lafudhi na matamshi sahihi, Bainisha maneno yenye makosa na ziandike upya sentensi hizo.
   a) Hata wenzetu waliosoma huendaga mjini.

   ______________________________

   b) Nimepata ujumbe wenye taharifa mbaya.

   ______________________________

   c) Kurara badala ya kufanya kazi kunasababisha maisha kuwa magumu.

   ______________________________

   d) Ama kweri erimu haina mwisho.

   ______________________________

   e) Ntoto wangu aumwa.

   ______________________________

   f) Zina makosa ziandike kwa ushahihi.

   ______________________________

   g) Mkuu wa shule alihairisha kikao

   ______________________________

   h) Hadisi tulizosimuliwa zinachekesha

   ______________________________

   i) Amenunua thamani za ndani

   ______________________________

   j) Kuku amekura majani

   ______________________________

7. Bainisha aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo
   i) Binti mrembo ametutembelea.

   ______________________________

ii) Viti vingi vimepotea

_______________________________________________

iii) Nyumbani kwao ni pazuri

_______________________________________________

iv) Kuku huyu ni wangu

_______________________________________________

v) Mwalimu Enjo anafundisha

_______________________________________________

8. We kama mwanafunzi wa kidato cha kwanza uliyesoma fasihi kwa ujumla, tumia mchoro kuonesha tanzu nne za fasihi simulizi na vipera vyake (vinne kwa kila utanzu)

9. (a) Bainisha taarifa tano zinazopatikana katika kamusi kuhusu kidahizo.

(b) Panga nmaneno yafuatayo kwa utaratibu wa kikamusi
Bata, uma, kimbia, chama, kingo, lima, kilimo, vema, wima, kimbilia

i. ______ vi. ______
ii. ______ vii. ______
iii. ______ viii. ______
iv. ______ ix. ______
v. ______ x. ______

10. Andika barua kwa dada yako mpendwa Embe Nyonyo ukimueleza:
    i. Maendeleo yako katika masomo
    ii. Kumuomba fedha sh. 25,000/- za kununua mahitaji ya shule

Wewe ni Nipe Nikupe mwanafunzi katika SHULE YA SEKONDARI SIHANGAIKI SLP 2314, GEITA.